

MAMLAKA YA MAPATO ZANZIBAR

TANGAZO LA NAFASI ZA AJIRA YA MUDA (INTERNSHIP)

Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA), ni Wakala Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Ukusanyaji na Usimamizi wa Mapato ya Kodi za ndani, ilioanzishwa kwa **sheria namba 11 ya mwaka 2022**.

ZRA, inatangaza nafasi sitini (60) za ajira ya muda (Internship) kwa ajili ya kusaidia shughuli za ukusanyaji Mapato kama ifuatavyo: -

NAFASI YA KAZI: MKUSANYAJI MAPATO

KITUO CHA KAZI: Unguja nafasi **50**, Pemba nafasi **10**

A. SIFA ZA WAOMBADI

- Awe na Shahada ya kwanza au elimu inayolingana nayo na kufaulu masomo ama ya Kodi, biashara, Uhasibu, Uanasheria, Uchumi, Teknolojia ya Habari na nyingine zinazofanana na hizo kutoka chuo kinachotambulika na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.
- Awe na uwezo wa kutumia Computer.

B. MUDA WA AJIRA

Kipindi cha **Miezi kumi na mbili (12)** baada ya kufunga Mkataba.

C. SIFA ZA JUMLA ZA WAOMBADI

- Awe na Kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi.
- Awe muadilifu na muaminifu.
- Awe na umri usiozidi miaka 30.
- Awe ni Mkazi wa Pemba, kwa Maombi ya nafasi za Pemba, na Mkazi wa Unguja kwa nafasi za Maombi ya Unguja.
- Awe na ufahamu wa maeneo ya Kituo cha kazi anachoomba.



1 Barabara ya Fumba, 71125 Mjini Magharibi,
Zanzibar
262 Kusini Pemba, Zanzibar Barabara ya Chake-Wete,

74206 Wara,



255-24-2233041
255-24-245255 (P)



zra@zanrevenue.org
SLP 2072, SLP 163 (P)



www.zanrevenue.org

D. MAJUKUMU YA KAZI

- i. Kufuatilia matumizi sahihi ya mashine za kutolea risiti za kielektroniki
- ii. Kusaidia uhamasishaji wa kudai risiti za kielektroniki kwa jamii. iii.
Kufuatilia walipakodi wasiowasilisha Ritani (non-fillers).
- iv. Kufuatilia walipakodi waliowasilisha Ritani na hawajafanya malipo (non-payers)
- v. Kufuatilia walipakodi wanaowasilisha Ritani zisizo na malipo (nil return).
- vi. Kufuatilia uwasilishaji wa ritani za malipo kwa wakati. vii.
Kufuatilia na kuwatambua wafanyabiashara wasiosajiliwa.
- viii. Kufanya uhakiki wa taarifa za usajili wa walipakodi kulingana na biashara zao.
- ix. Kufuatilia malalamiko ya mfumo wa VFMS kwa walipakodi na kuyapatia ufumbuzi ipasavyo.
- x. Kusaidia kufuatilia taarifa za madeni ya walipakodi. xi.
Kufuatilia taarifa za wakwepa kodi
- xii. Kushauri namna ya kuzuia mianya ya ukwepaji kodi **E**.

UTARATIBU WA KUWASILISHA MAOMBI.

Kwa waombaji wote wanatakiwa kuwasilisha barua ya maombi na kuambatanisha na vivuli vya taarifa zifuatazo: -

- 1) Vyeti vya kumalizia masomo.
- 2) Cheti cha kuzaliwa,
- 3) Kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi
- 4) Picha ya pasipoti iliyopigwa karibuni.
- 5) CV na majina mawili ya wadhamini wakuaminika

Maombi yote yawasilishwe kwa anuani ifuatayo:

**Kamishna Mkuu,
Mamlaka ya Mapato Zanzibar,
ZRA House Mazizini,
P.O. BOX 2072,
Fumba Road, 71125,
Urban West District,
ZANZIBAR**

Katika ofisi yake iliopo Mazizini Zanzibar kwa Upande wa Unguja, na kwa upande wa Pemba maombi yapelekwe katika ofisi ya Mamlaka ya Mapato Zanzibar iliopo Gombani Chake Chake Pemba.

Kwa muombaji yejote atakaewasilisha “Provisional result, Statement of result, Progressive reports” maombi yake hayatozingatiwa.

Maombi yataanza kupokelewa kuanzia tarehe 15/04/2024 hadi tarehe 19/04/2024 wakati wa saa kazi.